CHUO KIKUU CHA
SOKOINE CHA KILIMO

JARIDA

TOLEO MAALUMU LA MAONESHO YA WAKULIMA, WAFUGAJI NA WAVUVI

Ardhi ni Hazina

YALIYOMO

1 Waziri Mkuu akoshwa na teknolojia za kisasa katika kilimo zinazooneshwa na SUA Nanenane 2026

2 SUA yaibuka kidedea Nanenane, 2026

3 Waziri Kapinga avutiwa teknolojia na ubunifu wa kilimo wa SUA

4 Dkt. Kikwete aisifu SUA, afurahishwa na wanafunzi kujifunza kilimo

5 Utafiti wa kipekee wa SUA waitangaza Tanzania kimataifa

6 Mwenyekiti wa Baraza la SUA ahimiza tafiti na bunifu kuwafikia wananchi zaidi

7 Wanafunzi Mafiga waonesha mbegu bora za mpunga na mbinu rafiki za kudhibiti panya

8 Wakulima washauriwa kutumia teknolojia za kisasa kuongeza tija

9 SUA yaonesha teknolojia ya kutengeneza nyuzi kutoka majani ya nanasi

10 SUA yabuni mfumo wa AI wa kuhesabu vifaranga vya samaki

11 Mbegu mpya ya Maharage yatajwa kuongeza tija kwa wakulima

12 Wakulima watakiwa kutumia teknolojia ya Aquaponic kuongeza tija

13 Mfumo wa California Cage wafungua fursa ya kufuga kuku wengi katika eneo dogo

14 Wananchi wahimizwa kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa

15 Mafunzo ya SUA yawawezesha wajasiriamali kuongeza thamani ya mazao

16 Fahamu umuhimu wa kupima udongo kabla ya kuanza kilimo

17 Mchicha Lishe waelezwa kuwa chanzo bora cha virutubisho

19 Teknolojia ya kuzalisha malisho bila udongo yarahisisha ufugaji wenye tija

20 Maabara Tembezi yafikisha huduma za uchunguzi karibu na wananchi

21 SUA yaonesha namna malisho bora yanavyoweza kupunguza migogoro

22 SUA yahamasisha ulaji wa makundi sita ya vyakula kulinda afya

23 Elimu ya Amali SUA yaanza kuzaa matunda kwa wanafunzi wa Mafiga

24
- Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi atembelea Banda la SUA, Mbeya
- SUA inavyotumia bundi kulinda mashamba dhidi ya panya waharibifu

25 SUA yaongeza thamani ya mazao ya misitu kupitia Vuyisile Mini Furniture Factory

Waziri Mkuu akoshwa na teknolojia za kisasa katika kilimo kutoka SUA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa uwekezaji wake katika tafiti na teknolojia za kilimo zinazochangia kuongeza uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula na kuleta maendeleo katika sekta ya kilimo nchini.

Pongezi hizo alizitoa leo tarehe 4 Agosti, 2026, alipotembelea Banda la SUA katika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki ambapo alipata fursa ya kujionea na kupatiwa maelezo kuhusu teknolojia, ubunifu na tafiti mbalimbali zinazowasilishwa na Chuo katika maonesho ya mwaka huu.

Akiwa katika banda hilo Mhe. Dkt. Nchemba alisema SUA imeendelea kuwa kinara katika ubunifu na maendeleo ya teknolojia huku akisema juhudi za Chuo katika kuimarisha elimu ya vitendo ni muhimu kuelekea katika nchi inayojitegemea.

Alisema kuwa kuwaandaa wanafunzi wenye ujuzi wa vitendo ni hatua muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kwani taifa linahitaji wataalamu wabunifu na wenye uwezo wa kutumia maarifa yao kuleta mabadiliko chanya katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

SUA yaibuka kidedea Nanenane, 2026

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeibuka mshindi wa kwanza katika kundi la taasisi za mafunzo na utafiti na kushika nafasi ya tatu kwa jumla katika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki 2026, ikiwa ni matokeo ya ushiriki wake katika kuonesha tafiti, teknolojia, ubunifu na huduma mbalimbali zinazolenga kuongeza tija katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maeneo mengine ya maendeleo.

Akizungumza baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza (ICE) ambaye pia ni Mratibu wa Maonesho ya Nanenane kwa upande wa SUA, Dkt. Devotha Mosha, alishukuru kwa ushindi huo akisema mafanikio hayo ni motisha kwa Chuo kuendelea kujiandaa vizuri.

Aidha, Dkt. Devotha aliishukuru Menejimenti ya SUA kwa ushirikiano na uwezeshaji katika kufanikisha ushiriki wa Chuo kwenye maonesho hayo, pamoja na wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi na utoaji wa huduma.

Pia aliwashukuru wananchi na wadau mbalimbali waliotembelea mabanda ya SUA na kupata elimu, maarifa na taarifa kuhusu teknolojia na ubunifu unaozalishwa na Chuo.

Katika maonesho hayo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliibuka mshindi wa kwanza wa jumla huku mshindi wa pili ikiwa ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki 2026 yalifungwa rasmi Agosti 8, 2026 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, baada ya siku kadhaa za maonesho yaliyowakutanisha wakulima, wafugaji, wavuvi, watafiti, taasisi na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo.

Waziri Kapinga avutiwa teknolojia na ubunifu wa kilimo wa SUA

Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Judith Kapinga, alitembelea banda la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika Maonesho ya Nanenane yaliyoanza Agosti 1, 2026, na kujionea teknolojia mbalimbali za kisasa zinazolenga kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Akiwa katika banda hilo, Mhe. Kapinga alitembelea maeneo mbalimbali ya maonesho na kupata maelezo kuhusu teknolojia na ubunifu unaofanywa na watafiti wa SUA kwa ajili ya kuwasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi kuongeza tija, kuboresha uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa zao.

Waziri Kapinga alipokelewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Amandus Muhairwa, kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda.

Katika ziara hiyo, Mhe. Kapinga alijionea teknolojia zinazohusu uzalishaji wa mazao, ufugaji wa kisasa, uvuvi na uchakataji wa mazao, pamoja na bidhaa mbalimbali za kibunifu zinazotokana na tafiti zinazofanywa na chuo hicho. Aidha, alipata maelezo kutoka kwa wataalamu na watafiti kuhusu matumizi na manufaa ya teknolojia hizo kwa wazalishaji na jamii kwa ujumla.

Ushiriki wa SUA katika Maonesho ya Nanenane unaendelea kuwa jukwaa muhimu la kuunganisha tafiti, teknolojia na matumizi yake katika mazingira halisi ambapo kupitia maonesho hayo, chuo kinatoa elimu, ushauri wa kitaalamu na teknolojia kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wadau wengine, kwa lengo la kuongeza tija na kuchangia maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo nchini.

Dkt. Kikwete aisifu SUA, afurahishwa na wanafunzi kujifunza kilimo

Agosti 7, 2026, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alitembelea banda la SUA na kupokelewa na Menejimenti ya Chuo ikiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda.

Akiwa katika banda hilo, Dkt. Kikwete alipata maelezo ya jumla kutoka kwa Prof. Chibunda kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na SUA katika maeneo ya utafiti, ubunifu, teknolojia na utoaji wa elimu kwa wakulima, wafugaji na wadau wengine wa sekta ya kilimo.

Dkt. Kikwete ameipongeza SUA kwa kazi nzuri inayofanya katika kutoa elimu kwa wakulima pamoja na kuendeleza teknolojia zinazolenga kuongeza tija katika kilimo, mifugo na uzalishaji kwa ujumla.

Aidha, alifurahishwa na kuwepo kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mafiga wanaosoma mkondo wa amali ya kilimo, ambao walipata nafasi ya kumweleza shughuli mbalimbali za kilimo wanazojifunza na kuzifanya kwa vitendo.

Kuwepo kwa wanafunzi hao katika banda la SUA kunaonesha umuhimu wa kuwajengea vijana maarifa na ujuzi wa kilimo tangu wakiwa shuleni, ili kuwaandaa kutumia fursa zilizopo katika sekta hiyo na kushiriki katika maendeleo ya kilimo cha kisasa nchini.

Utafiti wa kipekee wa SUA waitangaza Tanzania kimataifa

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kufanya tafiti za kipekee zenye mchango mkubwa katika kutatua changamoto za afya na usalama duniani, hususan matumizi ya panya waliofunzwa kugundua kifua kikuu (TB) pamoja na mabomu yaliyotegwa ardhini.

Aliyasema hayo 08 Agosti, 2026 baada ya kutembelea banda la SUA katika Maonesho ya Nanenane. Prof. Kabudi alisema Tanzania ina sababu ya kujivunia utaalamu huo unaotekelezwa kupitia SUA, akieleza kuwa ni miongoni mwa ubunifu wa kipekee unaolitangaza Taifa kimataifa na kuonesha uwezo wa wataalamu wa Kitanzania kutoa suluhisho kwa changamoto zinazokabili mataifa mbalimbali.

Alisema uwezo wa panya hao kutambua sampuli za makohozi yenye vimelea vya Kifua Kikuu pamoja na kugundua mabomu ya ardhini ni teknolojia ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika kuokoa maisha ya watu na kurejesha maeneo yaliyokuwa hatarishi katika matumizi salama ya wananchi.

"Mimi nashukuru sana kwamba nimeona ni vyema nije hapa kwa sababu Tanzania tuna vitu vingi sana vya kipekee duniani lakini vingi havifahamiki, haya tunayoyaona hapa SUA ni fahari ya Tanzania na ni mchango mkubwa wa Tanzania kwa dunia," alisema Prof. Kabudi.

Alisema ingawa Tanzania imeendelea kufurahia amani na haina changamoto kubwa ya mabomu yaliyotegwa ardhini, utaalamu unaopatikana nchini umeweza kusaidia mataifa yaliyowahi kukumbwa na vita, yakiwemo Cambodia, Msumbiji na Angola.

"Nataka kusema kwamba, Baba wa Taifa ambaye ndiye aliyeanzisha safari ya kukifanya SUA kuwa chuo kamili, leo angekuwa hai na akaona haya ambayo SUA imewekeza katika kilimo, sayansi na utafiti, angefurahi sana," alisema Prof. Kabudi



Mwenyekiti wa Baraza la SUA ahimiza tafiti na bunifu kuwafikia wananchi zaidi

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Bw. Andrew William Massawe, alitembelea banda la SUA katika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki 2026, ambapo amejionea tafiti, teknolojia na bunifu mbalimbali zinazowasilishwa na Chuo kwa wananchi na wadau wa sekta ya kilimo.

Katika ziara hiyo, Bw. Massawe alipokea maelezo kutoka kwa wataalamu wa SUA kuhusu tafiti, teknolojia na bunifu zinazolenga kutoa suluhisho kwa changamoto zinazowakabili wakulima, wafugaji na wadau wengine wa sekta ya kilimo.

Baada ya kutembelea banda hilo, Bw. Massawe aliwapongeza wafanyakazi na wataalamu wa SUA wanaoshiriki katika Maonesho ya Nanenane kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwafikishia wananchi elimu, teknolojia na matokeo ya tafiti zinazofanywa na Chuo.

Alisisitiza umuhimu wa juhudi hizo kuendelea hata baada ya kumalizika kwa Maonesho ya Nanenane, huku akiitaka SUA kuongeza wigo wa kuwafikia wananchi ili tafiti na bunifu zinazozalishwa na Chuo zitumike zaidi katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii.

Alisema ni muhimu kuendelea kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na kuhakikisha maarifa yanayozalishwa kupitia tafiti za SUA yanawafikia wananchi wengi zaidi na kuleta matokeo chanya katika shughuli zao za uzalishaji na maendeleo kwa ujumla.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Raphael Chibunda, aliwapongeza wafanyakazi na wataalamu wa Chuo kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Maonesho ya Nanenane, akieleza kuwa juhudi zao zimeendelea kuitangaza SUA kupitia tafiti, teknolojia na bunifu zinazowasilishwa kwa wananchi.

Wanafunzi shule ya Sekondari Mafiga waonesha mbegu bora za mpunga na mbinu rafiki za kudhibiti panya

Mbegu bora za mpunga pamoja na mbinu rafiki kwa mazingira za kudhibiti panya ni miongoni mwa teknolojia zilizooneshwa na Shule ya Sekondari Mafiga katika Maonesho ya Nanenane.

Akizungumza na SUA Media katika maonesho hayo, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika mkondo wa amali, Stella Emmanuel, alisema teknolojia hizo zinalenga kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kupunguza uharibifu wa mazao mashambani.

Stella alisema miongoni mwa mbegu zinazooneshwa ni aina ya Mwangaza na Supa BC. Ameeleza kuwa mbegu ya Mwangaza ina uwezo wa kuvumilia ukame na kutoa mavuno mengi, hivyo kuwafaa wakulima wanaolima katika maeneo yenye upungufu wa mvua.

Aliongeza kuwa mbegu ya Supa BC inafaa kupandwa katika maeneo yenye maji mengi kwa kuwa ina uwezo wa kustahimili hali ya mafuriko. Sifa hiyo inawapa wakulima nafasi ya kupata mavuno mazuri hata katika maeneo yanayokumbwa na maji mengi.

Mbali na mbegu hizo, wanafunzi hao walionesha mbinu ya asili ya kudhibiti panya inayojulikana kama Trap Barrier System, mbinu ambayo hutumia nailoni kuzungushia eneo la mpunga ili kuzuia panya wasiingie shambani na kuwaelekeza katika mitego maalumu.

Stella alisema pia matumizi ya ndege aina ya bundi ni njia rafiki kwa mazingira ya kudhibiti panya, kwa kuwa bundi ana uwezo mkubwa wa kuona wakati wa usiku na kuwala panya wanaoingia mashambani na hivyo kusaidia kupunguza matumizi ya viuatilifu na kemikali zenye sumu ambazo zinaweza kuathiri mazingira na afya ya binadamu.

Wakulima washauriwa kutumia teknolojia za kisasa kuongeza tija

Wakulima nchini wameshauriwa kutumia teknolojia za kisasa za kilimo ili kuongeza uzalishaji, kuinua kipato na kuifanya sekta ya kilimo kuwa yenye tija zaidi.

Rai hiyo ilitolewa na Leonard Mwankemwa, Mhadhiri Msaidizi katika Idara ya Sayansi za Chakula ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), wakati wa Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki yanayofanyika mkoani Morogoro.

Akizungumza na SUA Media, Mwankemwa alisema SUA imeendelea kubuni na kutengeneza teknolojia mbalimbali za kisasa zinazolenga kurahisisha shughuli za kilimo, kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija kwa wakulima.

Alisema baadhi ya teknolojia hizo ni mashine ya kuchanganyia mbolea na virutubisho vya udongo (Soil Amendment Mixer); mashine ya kupandia mpunga kwa mistari miwili (Two-Row Rice Planter), inayopanda kwa nafasi ya sentimita 25; mashine ya kusaga na kukaanga mdalasini (Cinnamon Roasting Machine); mashine za kutengeneza matuta (Ridger Machine); pamoja na mashine yenye matumizi mbalimbali ya BOPI Mobile, inayoweza kufyeka nyasi na kuchakata mazao tofauti.

Teknolojia nyingine ni mashine ya kupanda bila kulima ardhi (Zero-Till Planter), ambayo husaidia kupunguza usumbufu wa udongo, kuhifadhi unyevunyevu na kupunguza muda na gharama za maandalizi ya shamba.

Aidha, Mwankemwa alisema SUA imebuni mifumo ya kisasa ya umwagiliaji inayofaa kutumika katika bustani, vitalu vya mahindi na mashamba ya mazao mengine yanayohitaji maji ya kutosha. Mifumo hiyo husaidia kutumia maji kwa ufanisi, kuhifadhi unyevunyevu wa udongo na kuchochea ukuaji mzuri wa mazao.

Mwankemwa amewahimiza wakulima kutembelea SUA ili kujifunza zaidi matumizi ya teknolojia hizo, namna zinavyofanya kazi na jinsi zinavyoweza kuwasaidia kuongeza uzalishaji, ubora na thamani ya mazao yao.

SUA yaonesha teknolojia ya kutengeneza nyuzi kutoka majani ya nanasi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeendelea kuonesha ubunifu katika Maonesho ya Nanenane 2026 kwa kuwasilisha teknolojia mbalimbali za ushonaji na utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na malighafi za asili, ikiwemo teknolojia ya kuzalisha nyuzi kutoka kwenye majani ya nanasi.

Akizungumza katika maonesho hayo, Mhadhiri wa SUA kutoka Idara ya Lishe na Stadi za Mlaji, Dkt. Zahara Majili, alisema miongoni mwa ubunifu uliowasilishwa mwaka huu ni teknolojia ya kuzalisha nyuzi kutoka kwenye majani ya nanasi, ambazo hutumika kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Alisema nyuzi hizo zinaweza kutumika kutengeneza mikoba, mikanda, mapambo ya mezani pamoja na bidhaa nyingine za matumizi ya nyumbani, hatua inayosaidia kuongeza thamani ya mabaki ya mimea ambayo mara nyingi hutupwa baada ya kuvuna matunda ya nanasi.

Dkt. Zahara alisema SUA pia inaonesha teknolojia ya kutengeneza rangi za asili zinazozalishwa kutoka kwenye mimea, ikiwemo manjano. Rangi hizo hutumika kutengeneza vitambaa vya batiki kwa njia rafiki kwa mazingira na salama kwa watengenezaji na watumiaji.

Aidha, alisema kuwa SUA kuna bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa kwa kutumia ngozi kwa ajili ya urembo, mavazi na mapambo ya ndani ambapo wananchi wanapaswa kutembelea ili kupata elimu zaidi kuhusu namna ya kutengeneza bidhaa hizo pamoja na fursa za ajira na biashara zinazopatikana katika sekta za ngozi, ushonaji na ubunifu wa mavazi.

SUA yabuni mfumo wa AI wa kuhesabu vifaranga vya samaki

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimebuni teknolojia ya akili unde (AI) ijulikanayo kama Tilapia Fingerling Counter, inayowezesha kuhesabu vifaranga vya samaki kwa kutumia simu ya mkononi kwa haraka na kwa usahihi.

Ubunifu huo unalenga kurahisisha zoezi la kuhesabu vifaranga na kupunguza changamoto zinazojitokeza wakati wa shughuli hiyo.

Akizungumza na SUA Media wakati wa Maonesho ya Nanenane, Mhadhiri Msaidizi kutoka Idara ya Uzalishaji wa Viumbe wa Majini na Malisho, Magoti Ernest, alisema mfumo huo unawasaidia wafugaji wa samaki kuhesabu vifaranga kwa muda mfupi na kuongeza uhakika wa idadi wakati wa kufanya biashara.

Ernest alieleza kuwa mfumo huo huchukua takribani dakika tano kukamilisha zoezi la kuhesabu vifaranga, hivyo kuokoa muda unaoweza kutumika katika shughuli nyingine za uzalishaji.

“Teknolojia hii inapunguza muda wa kazi, inaongeza usahihi wa hesabu na kumwezesha mfugaji kuendelea na shughuli nyingine kwa haraka,” alisema.

Aidha, alisema mfumo huo unapunguza matumizi ya nguvu kazi kwa kuwa unaweza kutumiwa na mtu yeyote mwenye simu ya mkononi. Pia unasaidia kupunguza vifo vya vifaranga vinavyoweza kutokea wakati wa kuhesabiwa kwa kutumia njia za kawaida.

Ernest alibainisha kuwa wazo la kuanzisha mfumo huo lilitokana na changamoto zilizokuwa zikiwakabili wafugaji katika kuhesabu vifaranga kwa usahihi na ufanisi.

Aliongeza kuwa kwa sasa mfumo huo umefikia kiwango cha usahihi cha takribani asilimia 88 na tayari unatumiwa na zaidi ya watu 50, ambao wameanza kunufaika nao katika shughuli zao za ufugaji wa samaki.

“Nawashauri wafugaji na wadau wengine wa sekta ya uvuvi na ufugaji wa samaki kutumia teknolojia hii, kwa kuwa maendeleo ya teknolojia yanaenda kwa kasi. Ubunifu huu utasaidia kutatua changamoto zinazoweza kuzuia maendeleo ya kilimo na kurahisisha shughuli za ufugaji wa samaki,” alisema.

Mbegu mpya ya Maharage yatajwa kuongeza tija kwa wakulima

Mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Mafiga iliyo chini ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kalunde Hamisi, amesema shule hiyo imeshiriki Maonesho ya Nanenane 2026, kwa kuonesha mbegu mpya za mazao zilizogunduliwa na watafiti wa SUA.

Kalunde alisema miongoni mwa mbegu hizo ni aina mpya ya maharage inayojulikana kwa jina la SUA Karanga iliyogunduliwa na Prof. Paul Kusolwa, ambayo imezalishwa kwa lengo la kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kupata mazao bora.

Alieleza kuwa maharage ya SUA Karanga yana sifa mbalimbali, ikiwemo uwezo wa kuvumilia magonjwa yanayoshambulia zao la maharage pamoja na kutoa mavuno mengi yakilinganishwa na baadhi ya aina nyingine za maharage.

Kalunde alisema mkulima anayefuata kanuni bora za kilimo anaweza kupata mavuno ya kati ya tani 1.5 hadi tani 3 kwa hekta moja baada ya kupanda mbegu hiyo.

Aliwashauri wakulima kutumia mbegu bora ya SUA Karanga ili kuongeza tija, kipato na faida katika kilimo cha maharage, huku akiwataka kupata ushauri wa kitaalamu kuhusu namna sahihi ya kuipanda na kuitunza.

Wakulima watakiwa kutumia teknolojia ya Aquaponic kuongeza tija

Wakulima wametakiwa kutumia teknolojia ya Aquaponic, mfumo unaounganisha ufugaji wa samaki na kilimo cha mboga, kwa kuwa unamwezesha mkulima kupata mazao zaidi ya moja kwa wakati mmoja huku akipunguza matumizi ya maji na gharama za uzalishaji.

Akizungumza katika Maonesho ya Nanenane, Mhadhiri Msaidizi kutoka Idara ya Sayansi ya Wanyama, Ukuzaji Viumbe Maji na Nyanda za Malisho katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Bi. Zipora Maiga, amesema teknolojia hiyo humwezesha mkulima kuzalisha samaki kwa ajili ya kupata protini pamoja na mboga za majani kupitia mfumo mmoja unaotumia rasilimali kwa ufanisi.

Bi. Maiga ameeleza kuwa uchafu unaozalishwa na samaki husafirishwa pamoja na maji kwenda kwenye mimea, ikiwemo mboga aina ya chainizi, ambako virutubisho vilivyomo hutumika kama mbolea ya asili inayosaidia mimea kukua vizuri na kuongeza uzalishaji.

Aidha, amesema mfumo huo hupunguza matumizi ya maji kwa kiasi kikubwa kwa kuwa maji huzungushwa ndani ya mfumo na kutumika kwa muda mrefu, tofauti na kilimo cha kawaida ambacho huhitaji maji mengi zaidi.

Ameongeza kuwa vifaa vinavyotumika kutengeneza mfumo huo vinapatikana kwa urahisi na vinaweza kuunganishwa na mkulima mwenyewe baada ya kupata maelekezo sahihi, jambo linalorahisisha matumizi ya teknolojia hiyo na kupunguza gharama za kuanzisha na kuendesha uzalishaji.

Mfumo wa *California Cage* wafungua fursa ya kufuga kuku wengi katika eneo dogo

Wafugaji wa kuku nchini wametakiwa kutumia mfumo wa kisasa wa ufugaji unaojulikana kama California Cage ili kuongeza tija, kupunguza gharama za uzalishaji na kuinua kipato chao.

Akizungumza na SUA Media katika Maonesho ya Nanenane, mtaalamu wa shamba kutoka Idara ya Sayansi za Wanyama, Ukuzaji Viumbe Maji na Nyanda za Malisho katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Bi. Hyasinta Minde, alisema mfumo huo unamwezesha mfugaji kufuga kuku wengi katika eneo dogo, hivyo kutumia nafasi kwa ufanisi na kurahisisha usimamizi wa kuku.

Alisema ili kuku wazalishe vizuri, ni muhimu kuwapatia chakula bora, maji safi na ya kutosha pamoja na mazingira mazuri yanayosaidia kupunguza msongo na hatari ya magonjwa.

Bi. Minde alieleza kuwa mfumo wa California Cage husaidia kupunguza maambukizi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na kugusana na kinyesi, kwa kuwa kuku hutunzwa katika nafasi maalumu na mazingira ya banda yanaweza kusimamiwa kwa urahisi zaidi.

Aidha, alisema mfumo huo huwezesha kuku kupata hewa ya kutosha na maji safi huku ukirahisisha usafi wa banda. Ameongeza kuwa kinyesi cha kuku kinaweza kutumika kama mbolea au kuvundikwa katika mazingira yanayofaa ili kuzalisha wadudu wanaoweza kutumika kama chanzo cha protini katika lishe ya kuku.

Pia alisema mfumo huo hurahisisha zoezi la kukusanya mayai na kupunguza uwezekano wa kuku kuyafikia na kuyaharibu au kuyala, jambo linalosaidia kupunguza upotevu wa uzalishaji.

Wananchi wahimizwa kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa

Wananchi wamehimizwa kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, hususan ugonjwa wa kutupa mimba (brucellosis) na kifua kikuu cha wanyama.

Wameshauriwa kuchukua tahadhari hizo hasa wakati wa kuhudumia mifugo ambapo uwepo wa vifaa mbalimbali vya kisasa vinatoa nafasi ya kujilinda.

Akizungumza katika Maonesho ya Nanenane Morogoro, Mteknolojia wa Maabara wa Mradi wa Afya Moja, Elimu na Ushirikiano wa Sekta za Umma na Binafsi (OHEPP), Amina Abdallah, alisema mradi huo unatekelezwa na SUA kwa ushirikiano na taasisi za Tanzania na Japani, kwa lengo la kuimarisha udhibiti wa brucellosis na kifua kikuu vinavyoweza kuambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Alisema katika maonesho hayo mradi unaonesha vifaa vya kukusanya na kusafirisha sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa maabara pamoja na teknolojia ya uhalisia pepe (Virtual Reality – VR), inayotumika kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna magonjwa hayo yanavyoambukizwa na jinsi ya kujikinga nayo.

Mafunzo ya SUA yawawezesha wajasiriamali kuongeza thamani ya mazao

Wajasiriamali wameendelea kunufaika na mafunzo yanayotolewa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), yanayolenga kuwajengea uwezo wa kuongeza thamani ya mazao kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na nafaka pamoja na mazao ya viungo.

Akizungumza na SUA Media, mjasiriamali kutoka Saadan Food Products, Grace Msongole, alisema mafunzo aliyoyapata yamekuwa chachu ya kujiajiri na kuboresha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zinazotokana na nafaka na viungo, ikiwemo tangawizi na iliki.

Alisema kupitia mafunzo hayo amejifunza mbinu za kuongeza thamani ya mazao, kuanzia hatua ya uchakataji wa mbegu hadi uzalishaji wa unga ulio tayari kutumika katika bidhaa mbalimbali. Kwa mujibu wa Msongole, ujuzi huo umemsaidia kuongeza ubora wa bidhaa zake na kuimarisha ushindani wake katika soko.

Aliwahimiza wakulima na wajasiriamali wengine kufika SUA ili kupata mafunzo kuhusu mbinu za kisasa za uchakataji wa nafaka na mazao ya viungo, hatua itakayowawezesha kuzalisha bidhaa bora zinazokidhi mahitaji ya soko na kuongeza kipato.

Kwa upande wake, Afisa Msimamizi wa Uhamishaji wa Teknolojia kutoka SUA, Lucy Madalla, alisema chuo hicho kinaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuwajengea uwezo wajasiriamali kupitia mafunzo yanayolenga kukuza ubunifu, kujiajiri na kuongeza fursa za kiuchumi.

Aliongeza kuwa SUA pia huwakutanisha wajasiriamali na wataalamu mbalimbali ili kujifunza teknolojia na mbinu mpya za kilimo na uchakataji wa mazao. Alisema hatua hiyo inachangia kuongeza tija katika uzalishaji, kuinua thamani ya mazao na kuboresha kipato cha wananchi.



Fahamu umuhimu wa kupima udongo kabla ya kuanza kilimo

Wakulima nchini wamehimizwa kuacha kufanya kilimo kwa kubahatisha na badala yake kupima udongo ili kufahamu afya yake, aina ya virutubisho vilivyopo na mazao yanayofaa kulimwa kwa lengo la kuongeza tija na kupunguza gharama za uzalishaji.

Wito huo ulitolewa na Fadhil Hussen, Mteknolojia wa Maabara ya Udongo kutoka Idara ya Sayansi za Udongo na Jiolojia, Ndaki ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), wakati akizungumza na SUA Media katika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki.

Hussen alisema katika maonesho hayo SUA imepeleka huduma za upimaji wa sampuli za udongo pamoja na elimu kuhusu namna sahihi ya kuchukua sampuli na kuiwasilisha maabara ili kupata matokeo sahihi yatakayomwezesha mkulima kufanya maamuzi bora ya uzalishaji.

Alieleza kuwa baadhi ya vipimo vya msingi vinatolewa bure katika banda la SUA, ikiwemo vipimo vinavyosaidia kubaini kiwango cha tindikali na virutubisho vinavyopatikana katika udongo.

“Wananchi waje SUA ili wapate elimu kuhusu afya ya udongo na namna ya kufanya kilimo chenye tija. Wakulima wasibahatishe; wapime udongo ili wafahamu mahitaji yake kabla ya kuanza uzalishaji,” alisema Hussen.

Mchicha Lishe waelezwa kuwa chanzo bora cha virutubisho

Mbegu ya mchicha lishe aina ya Amaranth ni miongoni mwa mazao yaliyooneshwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mafiga iliyo chini ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika Maonesho ya Nanenane.

Akizungumza katika maonesho hayo, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika mkondo wa amali ya kilimo, Mariam Abed, alisema mchicha huo una majani yenye virutubisho vingi vinavyosaidia kuimarisha afya ya mwili.

Mariam alisema aina hiyo ya mchicha ina uwezo wa kuvumilia baadhi ya magonjwa ya mimea, yakiwemo magonjwa ya ukungu, hivyo kumsaidia mkulima kupunguza uharibifu wa mazao shambani.

Alieleza kuwa mchicha huo hukomaa ndani ya siku 35 hadi 40 baada ya kupandwa, hali inayomwezesha mkulima kuvuna kwa muda mfupi na kuuza mazao yake sokoni.

Aliongeza kuwa mchicha huo unafaa kutumiwa na watoto, wazee pamoja na wanawake wajawazito kwa kuwa una virutubisho muhimu kwa mwili, huku akiwashauri wakulima kulima mbegu bora ili kupata mazao yenye tija na lishe bora.



HABARI PICHA

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akifuatilia bunifu mbalimbali zilizoandaliwa na Shule ya Sekondari Mafiga ya mkoani Morogoro wakati wa maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki 2026.

Teknolojia ya kuzalisha malisho bila udongo yarahisisha ufugaji wenye tija

Wakulima na wafugaji nchini wamehimizwa kutumia teknolojia ya kuzalisha malisho ya mifugo bila kutumia udongo, ili kuongeza tija katika ufugaji na kuhakikisha upatikanaji wa chakula bora na salama kwa mifugo.

Hayo yalisemwa na Afisa Mifugo Mfawidhi kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Bw. William Hoza, wakati wa Maonesho ya Nanenane.

Alisema teknolojia hiyo huwezesha uzalishaji wa malisho ndani ya muda mfupi wa takribani wiki moja, tofauti na kilimo cha kawaida kinachohitaji muda mrefu zaidi.

Bw. Hoza alisema mfumo huo hauna gharama kubwa za uzalishaji na husaidia kuboresha lishe ya mifugo, kwa kuwa malisho yanayozalishwa yana virutubisho muhimu, ikiwemo vitamini A, vinavyochangia ukuaji mzuri na kuongezeka kwa uzito wa mifugo.

Alieleza kuwa katika uzalishaji wa malisho hayo hakuna matumizi ya mbolea wala kemikali, hivyo mifugo ikiwemo kuku, bata na sungura hupata chakula salama.

Aidha, teknolojia hiyo ni suluhisho kwa wakulima na wafugaji wenye uhaba wa ardhi, kwa kuwa inawawezesha kuzalisha kiasi kikubwa cha malisho katika eneo dogo na ndani ya muda mfupi, hivyo kuongeza ufanisi wa shughuli za ufugaji.

Bw. Hoza alisema ili kupata malisho bora, ni muhimu kutumia mbegu zenye ubora, kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha pamoja na mwanga unaohitajika katika hatua zote za ukuaji.

Aliwataka wakulima na wafugaji kutembelea banda la SUA katika Maonesho ya Nanenane ili kujifunza kwa vitendo namna teknolojia hiyo inavyofanya kazi na faida zake katika kuongeza tija.



Maabara Tembezi yafikisha huduma za uchunguzi karibu na wananchi

Maabara Tembezi ya Jenomiki (Mobile Genomic Laboratory) ya Taasisi ya SACIDS ya Afya Moja (SACIDS Foundation for One Health) imekuwa miongoni mwa teknolojia zilizovutia wananchi na wageni waliotembelea Maonesho ya Nanenane 2026, kutokana na uwezo wake wa kufikisha huduma za kisasa za uchunguzi wa vimelea katika maeneo yenye viashiria vya milipuko ya magonjwa.

Akitoa maelezo ya teknolojia hiyo inayoratibiwa na Dkt. Edson Kinimi, Mhadhiri kutoka Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwa niaba ya Prof. Gerald Misinzo, alisema kwa zaidi ya muongo mmoja, taasisi hiyo imekuwa mstari wa mbele katika kufanya tafiti zinazozingatia dhana ya Afya Moja kwa kuwakutanisha wataalamu wa afya ya binadamu, afya ya wanyama, mazingira na teknolojia.

Tofauti na utaratibu wa kawaida wa kusafirisha sampuli kwa umbali mrefu hadi katika maabara kuu, Maabara Tembezi ya Jenomiki hupelekwa moja kwa moja katika eneo lenye viashiria vya mlipuko wa ugonjwa, hatua ambayo hupunguza muda wa kupata majibu ya vipimo kutoka siku kadhaa hadi saa chache na kuwezesha mamlaka kuchukua hatua za haraka za kulinda afya ya umma.

Maabara hiyo imeunganishwa na mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa, ikiwemo AfyaData na Afya Msafiri, pamoja na mifumo ya ufuatiliaji wa majanga na dharura za kiafya. Mifumo hiyo hupokea taarifa kutoka kwa jamii na vituo vya afya, kuzichambua na kusaidia kutoa tahadhari ya mapema kuhusu uwezekano wa kutokea kwa milipuko.

Dkt. Kinimi alisema teknolojia hiyo ina umuhimu mkubwa katika kuimarisha usalama wa afya, hasa kutokana na magonjwa mengi yanayoibuka ni ya zoonotiki, ambayo huambukizwa kati ya wanyama na binadamu. Mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la watu na mwingiliano kati ya binadamu, mifugo na wanyamapori vimeendelea kuongeza hatari ya kuibuka na kusambaa kwa magonjwa hayo.

Kupitia maabara hiyo, SACIDS imechangia katika ufuatiliaji na uchunguzi wa magonjwa mbalimbali, yakiwemo Marburg, UVIKO-19, Mpox, Dengue, Chikungunya, Homa ya Bonde la Ufa, Leptospirosis, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo pamoja na Homa ya nguruwe .

Pia hutumika kufuatilia usalama wa chanjo na kutoa ushahidi wa kisayansi unaosaidia Serikali kufanya maamuzi ya kudhibiti milipuko.

Popo wana mchango mkubwa katika uchavushaji wa mimea, usambazaji wa mbegu, urejeshaji wa misitu na udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao pamoja na mbu, hivyo kuwa sehemu muhimu ya mfumo wa ikolojia.

SUA yaonesha namna malisho bora yanavyoweza kupunguza migogoro

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kupitia Kitengo cha Malisho, kimeeleza kuwa kilimo cha malisho bora ya wanyama kinaweza kuwa suluhisho la kudumu la kupunguza migogoro inayojitokeza mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji nchini.

Akizungumza katika Maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyofanyika mkoani Morogoro, Ahmed Enock Amasha kutoka Kitengo hicho alisema kupitia teknolojia ya kuzalisha malisho ya kisasa katika maeneo madogo, wafugaji wanaweza kupunguza utegemezi wa kutangatanga kutafuta chakula cha mifugo.

Amasha alisema katika banda la Kitengo cha Malisho wanaonesha aina mbalimbali za malisho yenye tija ambayo wafugaji wanaweza kuyazalisha bila kuathiri shughuli nyingine za kilimo.

Alisema miongoni mwa malisho hayo ni jamii ya mikunde kama Alfaalfa na Russian Comfrey, ambayo yana kiwango kikubwa cha protini na virutubisho vinavyosaidia ukuaji na uzalishaji wa mifugo. Pia yapo majani tembo kama Local Napier na Giant Juncao ambayo yana uwezo wa kustahimili ukame na kutoa mavuno mengi.

Aina nyingine za malisho ni nyasi kama Rhodes, Brachiaria na Cenchrus ambazo zinaweza kulimwa, kukatwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kulisha mifugo, hususan wakati wa kiangazi ambapo upatikanaji wa malisho huwa mdogo. Kwa mujibu wa Amasha, Giant Juncao inaweza kutoa mavuno ya hadi tani 180 kwa mwaka kwa hekta moja na kuwa na protini inayoweza kufikia asilimia 18, hivyo kusaidia kuongeza uzalishaji wa mifugo ya maziwa na nyama.

“Kwa kutumia malisho haya, mfugaji anaweza kulisha mifugo bila kutoka nje ya shamba lake. Hii inapunguza migogoro na wakulima kwa sababu hakuna kutangatanga. Pia, malisho haya yanaweza kulimwa kibiashara na kuuzwa kwa wafugaji wengine,” alisema Amasha.

Aidha, aliwataka wafugaji kuwekeza zaidi katika kilimo cha malisho bora badala ya kuongeza idadi ya mifugo bila kuwa na uhakika wa chakula, akisisitiza kuwa ni bora kuwa na mifugo michache yenye tija kuliko kuwa na makundi makubwa yasiyo na faida.

SUA yahamasisha ulaji wa makundi sita ya vyakula kulinda afya

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kupitia Idara ya Lishe ya Binadamu na Sayansi za Mlaji, kilitoa elimu kwa wananchi kuhusu ulaji unaofaa kwa kuzingatia makundi sita ya vyakula, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mwongozo wa Chakula na Mlaji wa Tanzanaia Bara 2023.

Akizungumza na SUA Media katika banda la SUA kwenye Maonesho ya Nanenane 2026, Bi. Khadija Boi kutoka Idara hiyo alisema ulaji wa kiafya unahitaji mtu kupata vyakula kutoka katika makundi yote sita kila siku kwa uwiano unaofaa.

"Tunashauri wananchi kula kwa afya kwa kufuata makundi sita ya vyakula ili mwili upate virutubisho vinavyohitajika," alisema.

Alisema kundi la kwanza ni la vyakula vya nafaka, mizizi na ndizi za kupika, ambalo linashauriwa kuchukua asilimia 36 ya mlo. Vyakula hivyo ni pamoja na mahindi, mtama, mchele, ulezi, ngano, muhogo, ndizi za kupika, viazi vitamu, viazi vikuu na magimbi.

Vyakula vya jamii ya kunde vinashauriwa kuchukua asilimia 18 ya mlo, vikiwemo maharage, njegere, karanga, mbaazi, kunde, njugu mawe na soya.

Vyakula vya asili ya wanyama vinapaswa kuchukua asilimia 10 na vinajumuisha nyama, mayai, maziwa, samaki, dagaa, kuku na wadudu wanaoliwa kama senene na kumbikumbi.

Kwa upande mwingine, matunda yanashauriwa kuchukua asilimia 17 ya mlo na mbogamboga asilimia 17. Matunda hayo ni pamoja na maembe, ndizi mbivu, papai, mapera, machungwa, nanasi, pesheni na parachichi, huku mbogamboga zikijumuisha mchicha, kisamvu, matembele, bamia, karoti, nyanya, matango, mlenda, maboga na biringanya.

Mafuta salama yanapaswa kuchukua asilimia mbili ya mlo hivyo wananchi wanashauriwa kutumia mafuta kwa kiasi na kuchagua vyanzo salama kama mafuta ya alizeti, nazi, mawese na mbegu mbalimbali zinazotoa mafuta.

Bi. Khadija alisema wananchi wanaotembelea banda hilo hupimwa uzito na urefu na kupewa ushauri wa lishe kwa kuzingatia vipimo hivyo pamoja na umri wao.

Elimu ya Amali SUA yaanza kuzaa matunda kwa wanafunzi wa Mafiga

Utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Amali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) umeanza kuonesha matokeo chanya kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mafiga, ambao wanapata fursa ya kujifunza kwa vitendo katika maeneo mbalimbali ya kilimo na ufugaji.

Akizungumza na SUA Media, Dkt. Hamidu Khalfan, Mtafiti na Msimamizi wa Elimu ya Amali kutoka Shule Kuu ya Elimu ya SUA, alisema wanafunzi wa shule hiyo wameanza kutumia maarifa na ujuzi wanaoupata katika shughuli za uzalishaji wa mazao, hususan kilimo cha mboga na kilimo cha mjini.

Alisema mafunzo hayo yanawawezesha wanafunzi kushiriki katika hatua mbalimbali za uzalishaji, kuanzia upandaji wa miche, utunzaji na ukuzaji wa mimea hadi uvunaji, huku wakijifunza pia matumizi ya teknolojia za kisasa za kilimo.

Dkt. Khalfan alisema miongoni mwa teknolojia wanazofundishwa ni mfumo wa umwagiliaji kwa njia ya matone pamoja na mbinu mbalimbali za uvunaji na uhifadhi wa maji kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Alieleza kuwa elimu hiyo inalenga kuwawezesha wanafunzi kuunganisha maarifa wanayopata darasani na ujuzi wa vitendo, ili waweze kuyatumia katika maisha yao ya kila siku na kujiandaa kwa fursa mbalimbali za ajira, kujiajiri na kuendelea na masomo.

Kwa mujibu wa Dkt. Khalfan, SUA inatekeleza elimu ya amali kupitia mikondo mbalimbali inayohusisha uzalishaji wa mazao, uendeshaji wa vitalu vya mimea, bustani za mazao ya chakula na maua, pamoja na ufugaji wa wanyama kwa kuzingatia mbinu bora za ufugaji, afya ya mifugo na matumizi ya teknolojia za kisasa.

Alisema Shule Kuu ya Elimu ya SUA imepewa jukumu la kuilea na kuiwezesha Shule ya Sekondari Mafiga katika utekelezaji wa elimu hiyo, hatua inayowapa wanafunzi mazingira mazuri ya kujifunza kupitia shughuli halisi za uzalishaji.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi atembelea Banda la SUA, Mbeya

Rasi wa Kampasi ya Mizengo Pinda, Prof. Anna Sikira, alimpokea Katibu Tawala wa Mkoa wa Katavi, Mhe. Albert Msovela alipotembelea banda la kampasi hiyo katika Maonesho ya Nanenane 2026 yanayofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.

Katika ziara hiyo, Mhe. Msovela alijumuika na wananchi pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo waliofika bandani hapo kupata elimu, kujifunza na kujionea teknolojia pamoja na ubunifu wa kitaaluma na kitafiti unaotolewa na Kampasi ya Mizengo Pinda.

Prof. Sikira alimweleza Katibu Tawala kuhusu jitihada zinazofanywa na kampasi hiyo katika kuendeleza sekta ya kilimo, ufugaji, na hifadhi ya mazingira, pamoja na kuwajengea uwezo wanafunzi na jamii kwa ujumla ili kuongeza tija na thamani katika uzalishaji.

SUA inavyotumia bundi kulinda mashamba dhidi ya panya waharibifu

Licha ya dhana iliyopo kumhusu ndege bundi, bado umuhimu wake umekuwa mkubwa kwa jamii ambapo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba alielezwa na SUA kuwa bundi amekuwa kiungo muhimu kati ya mkulima na mazao yake.

Utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo umemwelezea bundi kuwa ana mchango wa kudhibiti panya waharibifu wa mazao mashambani.

Teknolojia hiyo ilionyeshwa kwenye maonesho ya Nanenane 2026 mbele ya Waziri Mkuu, Dkt. Nchemba, ambapo alielezwa namna bundi anavyoweza kutumika kama njia rafiki ya mazingira katika kupunguza hasara kwa wakulima.

Dk Nchemba alisema jamii imekuwa ikimpa bundi sifa mbaya kwa muda mrefu, licha ya kuwa ndege huyo ana faida kubwa katika kulinda mashamba dhidi ya panya wanaoshambulia mahindi, mpunga na mazao mengine.

“Leo ndiyo mara yangu ya kwanza kumuona bundi ana kwa ana. Kumbe huyu ndege ambaye jamii imekuwa ikimpa sifa mbaya ana faida kubwa kwa wakulima. Hii ni teknolojia nzuri inayostahili kuenezwa,” alisema.

Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema bundi ni miongoni mwa njia salama za kudhibiti panya waharibifu kwa kuwa husaidia kupunguza matumizi ya sumu ambazo zinaweza kuathiri afya ya binadamu na mazingira.

SUA yaongeza thamani ya mazao ya misitu kupitia Vuyisile Mini Furniture Factory

Kiwanda cha Vuyisile Mini Furniture Factory cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kilichopo Kampasi ya Solomon Mahlangu, Mazimbu mkoani Morogoro, kimeendelea kuongeza thamani ya mazao ya misitu kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali za samani, zikiwemo madawati na viti kwa ajili ya shule na taasisi, pamoja na kutoa huduma za uchakataji na ukaushaji wa mbao kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Akizungumza na SUA Media, Mhadhiri Msaidizi kutoka Idara ya Uhandisi Misitu na Sayansi za Mazao ya Misitu, Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii, SUA, Mbonea Mweta, alisema kiwanda hicho kina zaidi ya mashine 60 zinazowezesha kutekeleza hatua mbalimbali za uzalishaji, kuanzia kuchana magogo, kukausha mbao, kuranda na kugereza hadi kufanya umaliziaji wa samani.

Alisema uwezo huo unakiwezesha kiwanda kuzalisha bidhaa zenye ubora na uimara kulingana na mahitaji ya wateja.

"Kiwanda chetu kinatengeneza bidhaa mbalimbali za samani, ikiwemo madawati na viti kwa ajili ya shule na taasisi mbalimbali. Pia tunatoa huduma ya ukaushaji wa mbao, jambo ambalo ni muhimu katika kuhakikisha mbao zinakuwa katika hali nzuri kabla ya kutumika kutengeneza bidhaa," alisema Mweta.

Katika kuendeleza matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, SUA kupitia Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii pia imeanzisha mradi wa majaribio wa tanuri la kukausha mbao kwa kutumia nishati yajua.

Teknolojia hiyo inalenga kupunguza utegemezi wa vyanzo vingine vya nishati, zikiwemo umeme na mafuta ya dizeli, huku ikisaidia kupunguza gharama za ukaushaji wa mbao na kuchangia katika utunzaji wa mazingira.

Mweta alisema matumizi ya teknolojia hizo yanaonesha namna SUA inavyotumia elimu, utafiti na ubunifu kuongeza thamani ya mazao ya misitu, kuboresha ubora wa bidhaa za mbao na kutoa huduma zinazoweza kunufaisha taasisi, wazalishaji na wananchi kwa ujumla.

HABARI PICHA

Mwanafunzi wa Stashahada ya Uzalishaji Mazao na Utunzaji Mary Sharon Boi akiwapa maelezo wageni waliofika katika Banda la SUA wakati wa maonesho ya Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ili kujifunza kuhusiana na teknolojia mbalimbali.



Afisa Udahili Bw. Abel Lugimba akiwaelekeza wazazi na walezi waliofika katika banda la SUA maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya ili kufahamu programu mbalimbali zinazotolewa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.



Jarida limeandaliwa na:
Kitengo cha Mawasiliano na Masoko
S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania
Simu: 255-023-2640006/7/8/9,
Baruapepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz